

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI

TE. No. 028 2802535  
Fax Na. 028 2802535  
E-mail address:  
kummnicipal@yahoo.com



Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa  
Halmashauri ya Manispaa,  
S.L.P 44,  
KIGOMA.

TAREHE: 08/05/2020

## TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji inapenda kuwaalika Wafanyabiashara, Watu binafsi, Wajasiliamali, Makampuni na mawakala wa kampuni za usafirishaji wenye nia na uwezo wa kupanga katika jengo la kuchakatia chakula cha kuku, Mgahawa, vibanda/ vyumba vya biashara/kukatia tiketi ndani ya stendi ya mabasi Masanga na soko la Nazareth, watume maombi yao kwa zabuni zifuatazo:-

NAMBA YA ZABUNI	AINA YA ZABUNI	GHARAMA YA MAOMBI KWA KILA ZABUNI	WANAOSTAHLI
1.LGA/042/2020/2021 /NC/01	Upangishaji wa vibanda/vyumba vya kukatia tiketi stendi ya mabasi Masanga.	TZS 30,000/=	Makampuni na mawakala wa kampuni za usafirishaji.
2.LGA/042/2020/2021/NC/02	Upangishaji wa vibanda/vyumba vya biashara soko la Nazareth	TZS 20,000/=	Makampuni, waja siliamali, ushirika, vikundi na watu binafsi.
3.LGA/042/2020/2021/NC/03	Upangishaji wa jengo la kuchakatia chakula cha kuku Kibirizi.	TZS 50,000/=	Makampuni, waja siliamali, ushirika, vikundi na watu binafsi.
4.LGA/042/2020/2021/NC/04	Upangishaji wa Mgahawa ndani ya stendi ya mabasi Masanga.	TZS 30,000/=	Makampuni, waja siliamali, ushirika, vikundi na watu binafsi .

A/042/2020/2021/NC/05	Upangishaji wa Mgahawa/Canteen ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji	TZS 30,000/=	Makampuni, waja siliamali, ushirika, vikundi na watu binafsi.
6.LGA/042/2020/2021/NC/06	Upangishaji wa chumba cha ("Stationery") ndani ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji	TZS 20,000/=	Makampuni, waja siliamali, ushirika, vikundi na watu binafsi.

Mwombaji anatakiwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:-

1. Kivuli cha Leseni ya zabuni husika.
2. Kivuli cha Cheti cha usajili (Certificate of Registration).
3. Kivuli cha Utambulisho wa mlipa kodi (FIN namba au VAT).
4. Aweke stakabadhi halisi ya malipo ya maombi husika.
5. Hati halisi ya uthibitisho wa uwakilishi wa ki-sheria (Power of attorney) kwa Makampuni tu.
6. Kivuli cha Hati ya kiapo (Affidavit form) kutoka Mahakamani kuwa mpangaji/mwombaji si mtumishi wala diwani wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji.
7. Kivuli cha taarifa za kibenki (Bank statements) za miezi mitatu inayoishia **29 February, 2020.**
8. Kivuli cha Taarifa za Kampuni (Company Profile) kwa makampuni tu.
9. Mdhamini mmoja kati ya wadhamini awe na kampuni ya usafirishaji na agonge muhuri wa Kampuni husika (Kwa waombaji wa vibanda vya kukatia tiketi stendi ya mabasi Masanga)

**NB:** Mwombaji atakayeshinda zabuni atapeleka kodi kila mwanzo wa mwezi katika Benki ya NMB (**Own Source Collection Account no: 51610000197**)

Mpangaji atatakiwa kupeleka kodi yote kwa mwezi. (kama huna uhakika wa kulipa kodi iliyotajwa usiombe chanzo husika).

#### **MASHARTI KWA MWOMBAJI:**

1. Mtu, Taasisi, Kampuni, Umoja, Kikundi au shirika lolote ambalo lilishawahi kupanga jengo la Manispaa ya Kigoma/Ujiji na **KUSHINDWA** kulipa kodi kwa mujibu wa Mkataba au kuvunja masharti yoyote ya mkataba kama vile kufanya udanganyifu **HARUHUSIWI/HAIRUHUSIWI/HIAURUHUSIWI/HAKIRUHUSIWI** kuomba kuwa Mpangaji.
2. Mshindi wa Zabuni husika atawajibika kufanya usafi wa eneo la kazi na kupeleka takataka eneo la kukusanyia taka
3. Mwombaji anaweza kuomba zabuni moja au zaidi.
4. Mwombaji ataje kodi/gharama atakayolipia kwa mwezi.

Mwombaji atakayeshinda zabuni atatakiwa kuweka dhamana (bond) kiasi sawa na kodi ya miezi mitatu (3) kabla ya kuanza kupanga ambayo mpangaji atarudishiwa baada ya ukomo wa mkataba endapo atakuwa hana deni lolote au uharibifu wowote. Au anaweza kuweka dhamana ya hati original ya nyumba, udhamini wa benki (bank guarantee). Mpangaji hatokabidhiwa chamba bila ya kuweka dhamana (bond).

6. Viwango vilivyopangwa vya fedha vinaweza kubadilika muda wowote kulingana na mabadiliko ya sheria mpya au kutokana na maelekezo ya serikali.
7. Mpangaji atakuwa na wajibu wa kutoa taarifa za changamoto anazokutana nazo kwa meneja wa chanzo husika na kwa Idara ya Fedha inapohitajika.
8. Mpangaji atatakiwa kulipia kodi ya pango kila mwanzo wa mwezi na anaweza kulipia mwezi mmoja au miezi mitatu mitatu kwa kuchukua Control number kwenye ofisi ya mapato ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.
9. Mwombaji atatakiwa kujaza taarifa zote vizuri katika zabuni anayoomba.
10. Mwombaji aoneshe waziwazi Makazi/ofisi yake ilipo na uzoefu wa kazi anayoomba (Kwa vibanda vya kukatia tiketi).
11. Kila mwombaji atalipa ada ya maombi ya zabuni ambayo haitarudishwa na kila ombi ni zabuni inayojitegemea na italipiwa kiasi cha ada kilichoainishwa katika **akaunti na. 51610000197 NMB** kwa jina la Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji baada ya kupewa **Control Number** inayotolewa katika kitengo cha Mapato ndani ya Manispaa
12. Watakaopata zabuni watatakiwa kuingia mkataba na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.
13. Bodi ya zabuni haitalazimika kukubali zabuni ambayo kodi yake iko juu au chini sana. (Atakayekidhi vigezo vya sheria ya manunuzi ndiye atakayepewa kibanda na Bodi ya zabuni).
14. Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha zikiwa ni **“ORIGINAL MOJA NA COPY MBILI”** (kwa Lakiri). Juu ya bahasha ioneshe aina ya zabuni na namba ya zabuni. Zabuni zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,**

**Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji,**

**S.L.P. 44, KIGOMA**

15. Kwa maelezo zaidi kuhusiana na zabuni hizi, fika katika Ofisi za Halmashauri ya Manispaa zilizopo eneo la Mnarani muone Katibu wa Bodi ya Zabuni.
16. Makabrasha ya zabuni yanapatikana katika ofisi ya Kitengo cha Manunuzi (PMU) ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.
17. Vigezo vya tathmini ya zabuni zote ni kama ilivyoainishwa kwenye tangazo pamoja na kwenye nyaraka za kila zabuni.

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya zabuni hizo ni **Alhamisi tarehe 21 Mei, 2020** ambayo ndiyo itakuwa siku ya ufunguzi wa zabuni hizo saa 5:00 Asubuhi katika ukumbi wa **Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji**. Mwombaji au mwakilishi wake wanakaribishwa katika ufunguzi wa zabuni hizo.

  
.....  
**MWALWA S. PANGANI**

**MKURUGENZI WA MANISPAA  
KIGOMA/UJJI.**

**MKURUGENZI WA MANISPAA  
KIGOMA/UJJI**